

**SHAYKH AL-
ALBAANIY -
MWANACHUONI
WA KARNE**

**Al-Imaam, Al- Muhadith, Shaykh
Muhammad Naaswirud-Diyn Al-
Albaaniy**

1332H-1420H - 1914M-1999M

**Abu 'Abdillaah Muhammad
Saalim Sa'iyd Baawazir**

Yaliyomo

| | |
|---|----|
| Utangulizi..... | 2 |
| Jina Lake Na Familia Yake..... | 7 |
| Kumbukumbu Za Ajabu..... | 8 |
| Kuzaliwa Na Kukua Kwake..... | 8 |
| Kujifunza Kwake Elimu Ya Hadiyth | 9 |
| Wanafunzi Wake Maarufu | 11 |
| Vitabu Vyake | 12 |
| Kueneza Kwake Elimu | 14 |
| Safari Zake..... | 16 |
| Upinzani | 18 |
| Uhusiano Wake Na Wanachuoni | 20 |
| Fadhila Na Mema Yake..... | 21 |
| Imaam Abu Haniyfah (رحمه الله) | 22 |
| Imaam Maalik (رحمه الله)..... | 23 |
| Imaam Ash-Shaafi'iy (رحمه الله)..... | 23 |
| Imaam Ahmad bin Hanbal (رحمه الله)..... | 24 |
| Elimu Yake Na Athari Yake Kwa Watu | 27 |
| Kipindi Cha Mwisho Cha Maisha Yake | 30 |
| Kifo Chake Na Jinsi Kilivyoathiri Ummah..... | 30 |
| Sifa Njema Na Heshima Walizotoa Wanachuoni Kwake..... | 31 |
| Shaykh 'Abdul-'Aziyz Bin Baaz [Aliyekuwa Mufti Wa Saudi Arabia] (رحمه الله) | 31 |
| Mwanachuoni Shaykh Muhammad Ibn Swaalih Al-'Uthaymiyn (رحمه الله) | 32 |
| Mwanachuoni Mfasiri Shaykh Muhammad Al-Amiyn Ash- Shanqiytwiy (رحمه الله)..... | 33 |
| Shaykh 'Abdul-Muhsin Al-'Abaadiy (الله حفظه)..... | 33 |
| Shaykh 'Abdullah Al-'Ubaylaan 'Abaadiy (الله حفظه) | 33 |
| Mufti Wa Zamani Wa Saudia Mwanachuoni Shaykh Muhammad Bin Ibraahiym Aal Shaykh (رحمه الله) | 34 |
| Mwanachuoni Shaykh Zayd Bin Fayyaadh (رحمه الله)..... | 34 |
| Mwanachuoni Shaykh Muqbil Al-Waadi'iy (رحمه الله)..... | 35 |
| Mwanachuoni Wa Misr Muhibud-Diyn Al-Khatwiyb (رحمه الله)..... | 35 |

| | |
|---|----|
| Mwanachuoni Wa Hadiyith India, Shaykh ‘Abdus-Swamad Sharafud-Diyn (رحمه الله)..... | 36 |
| Mwanachuoni Hamuud Bin ‘Abdillaah At-Tuwayjiriy (رحمه الله) | 36 |
| Profesa Amiyn Al-Misriy (رحمه الله) Aliyekuwa Mkuu Wa Kitengo Cha Masomo Ya Juu Katika Chuo Kikuu Cha Kiislam | 36 |
| Waliomsifu Baada Ya Kufa Kwake Ni:..... | 36 |
| Waziri Wa Masuala Ya Kiislamu, Al-Awqaaf, Ulinganio Na Uongozi Shaykh Swaalih Bin ‘Abdil-‘Aziyz Bin Muhammad Aali Shaykh..... | 37 |
| Katibu Mkuu Wa Shirikisho La Ulimwengu Wa Kiislamu Huko Makkah Al-Mukarramah Shaykh Dkt. ‘Abdullah Bin Swaalih Al-‘Ubayd..... | 37 |
| Tume Ya Kudumu Ya Tafiti Za Kitaaluma Na Utoaji Fatwa Saudi Arabia..... | 38 |
| Tenzi Kumhusu Shaykh Al-Albaaniy | 39 |
| Tanbihi Kutoka Kwa Mwandishi Wa Historia Hii | 42 |
| Mitandao Iliyoundwa Kwa Ajili Ya Kueneza Elimu Shaykh Al-Albaaniy (رحمه الله) | 42 |

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Utangulizi

Hakuna shaka yoyote kwamba, hakika shukrani zote zinamstahikia Allaah. Tunamhimidi, tunaomba msaada Kwake, na tunaomba maghfira. Tunaomba hifadhi kwake Allaah kutokana na maovu ya nafsi zetu, na makosa ya matendo yetu. Yeyote Allaah Anayemuongoza, hakuna wa kumpotosha, na yeyote Allaah Anayempotosha, hakuna wa kumuongoa. Ninashuhudia pia kwamba hakuna yeyote anayestahiki kuabudiwa isipokuwa Allaah, na ninashuhudia kwamba Muhammad (صلى الله عليه وآله وسلم) ni mjumbe na Mtume Wake.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ حَقَّ تَقَاتِهِ وَلَا تَمُوتُنَّ إِلَّا وَأَنْتُمْ مُسْلِمُونَ ﴿١٠٢﴾

{{Enyi mlioamini! Mcheni Allaah kama ipasavyo kumcha; wala msife isipokuwa mmekwishakuwa Waislamu kamili.}}¹

يَا أَيُّهَا النَّاسُ اتَّقُوا رَبَّكُمُ الَّذِي خَلَقَكُمْ مِنْ نَفْسٍ وَاحِدَةٍ وَخَلَقَ مِنْهَا زَوْجَهَا وَبَثَّ مِنْهُمَا رِجَالًا كَثِيرًا وَنِسَاءً ۚ وَاتَّقُوا اللَّهَ الَّذِي تَسَاءَلُونَ بِهِ وَالْأَرْحَامَ ۚ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلَيْكُمْ رَقِيبًا ﴿١﴾

{{Enyi watu! Mcheni Mola wenu Ambaye amekuumbeni katika nafsi (asli) moja. Na Akamuumba mkewe katika nafsi ile ile. Na Akaeneza wanaume wengi na wanawake kutoka katika wawili hao. Na mcheni Allaah ambaye kwaye mnaombana. Na (mwatazame) jamaa. Hakika Allaah ni Mlinzi juu yenu (anayaona kila mnayoyafanya).}}²

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَقُولُوا قَوْلًا سَدِيدًا ﴿٧٠﴾ يُصْلِحْ لَكُمْ أَعْمَالَكُمْ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ ۗ وَمَنْ يُطِعِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ فَازَ فَوْزًا عَظِيمًا ﴿٧١﴾

{{Enyi mlioamini! Muogopeni Allaah na semeni maneno ya haki. Atakutengenezeeni vizuri vitendo vyenu na Atakusameheni madhambi yenu; na anayemtii Allaah na Mtume Wake, bila shaka amefanikiwa mafanikio makubwa.}}³

¹ Al-'Imraan: 102

² An-Nisaa: 1

³ Al-Ahzaab: 70-71

Kwa hakika, maneno bora ya kweli ni Maneno ya Allaah, na uongofu bora ni uongofu wa Muhammad (صلى الله عليه وآله وسلم). Mambo maovu kabisa ni yale ya kuzusha, na kwa kila jambo jipya lililoanzishwa ni uzushi, na kwa kila uzushi ni upotofu, na upotofu unapelekea kuingia Motoni.

Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema:

“Kwa hakika, Wanachuoni ni warithi wa Mitume, na Mitume hawakuacha nyuma dinaar wala dirham kurithiwa. Isipokuwa, wameacha nyuma elimu ili kuweza kurithiwa, na yeyote anayechukua kutoka humo amepata manufaa makubwa mno.”⁴

“Ilmu hii (Dini) itabebwa na watu wenye kuaminika katika kila kizazi. Wakipinga *tahriyf* (madai ya kizushi) ya wale wanaovuka mipaka, madai ya uongo ya waongo, na wakipinga *ta-awiyl* (upindujaji tafsiri) za wajinga.”⁵

“Allaah Atamuinua katika jamii hii mwishoni mwa kila miaka mia moja mtu ambaye ataihuisha Dini yake.”⁶

Hakika Allaah (سبحانه وتعالى), Ambaye yametakasika majina Yake, kahusisha viumbe Vyake kwa kuwepo wale vipenzi kabisa. Akawaongoza katika Iymaan, Akawajaalia wawe na fadhila kubwa kwa walimwengu kwa kuwapa elimu ya Kitaab (Qur-aan) na Hikmah (Sunnah). Akawapa elimu ya shari’ah ya Dini Yake, Akawaruzuku upambanuzi wa ufasiri na ufahamu wa makusudio ya maandiko. Akawafadhalisha juu ya Waumini wote katika kila zama na kila eneo.

Historia ya Uislamu inasimama kama ni shahidi wa Wanachuoni wengi wakubwa wakubwa, watengenezaji na waitaji wa njia ya Allaah; wale ambao wamefuata nyayo za *Salafus-Swaalih* (wacha Mungu wa kale)

⁴ Kipande cha sehemu refu ya *Hadiyih* iliyosimuliwa na Abu Daawud (3641 & 3642), at-Tirmidhiy (2682), Ibn Maajah (223), na Ibn Hibbaan (88), na al-Albaaniy akaithibitisha kwamba ni sahihi ndani ya kitabu chake cha *Sahihy at-Targhiyb wa-Tarhiyb* (70).

⁵ Imesimuliwa na al-Bayhaqi na kusahihishwa na Shaykh al-Albaaniy ndani ya *Mishkaat*, namba 248.

⁶ Abu Dawud (3/4278), al-Haakim, at-Twabaraaniy ndani ya *al-Awsatw*. Imesahihishwa na al-Albaaniy ndani ya *as-Swahiyhah* (2/150))

katika *iymaan* na matendo, katika kumuitikia Allaah na kuweka vipaumbele kwenye maisha; katika ushujaa na ujasiri, katika hatari na jitihada na katika kujitoa muhanga wa maisha yao yote kwa moyo wote kwa ajili ya shughuli ambazo ni faida kwa ajili ya siku ya *Qiyaamah*.

Miongoni mwa Wanachuoni waliopewa Tawfiyq na Allaah na kuongozwa katika elimu na Iymaan na katika walioruzukiwa neema kubwa ya kuwa sababu ya elimu ya Hadiyth kupendwa na kujulikana zaidi na hata kuenea katika Ummah kwa mchango wake mkubwa katika fani hiyo, ni Imaam, Muhaddith, al-'Allaamah, Shaykh Muhammad Naaswirud-Diyn al-Albaaniy. Mwanachuoni huyu alikuwa bahari ya Hadiyth na Hoja katika mjadala na mtafiti, mpembuzi, mchambuzi, na hoja katika fani ya Hadiyth na istilahi zake.

Nimemchagua Mwanachuoni huyo kuandika historia yake kwa ufupi pamoja na kwamba kuna Wanachuoni wengi wa Ahlus Sunnah wal Jama'aah wakubwa wenye nafasi tukufu na elimu nyingi na mchango mkubwa, ila Imaam huyu ni katika Wanachuoni wachache sana walioacha taathira kubwa sana katika karne ya 20 na 21 na ataendelea kuacha taathira kubwa hadi karne zijazo kutokana na vitabu na kazi nyingi alizoacha nyuma yake ambazo zinaendelea kunufaisha na kutumika kila kukicha.

Katika Wanachuoni walioacha taathira kubwa zama na zama na taathira yake inayoendelea daima katika kila kizazi karne kwa karne, ni Imaam, Shaykh al-Islaam Ibn Taymiyyah (رحمه الله). Imaam huyu hatoweza kusahaulika kwa bahari na hazina ya elimu aliyoiacha na mchango mkubwa wa kusimamisha Dini hii na kuihuisha na kupigana Jihaad ya kusimamisha Sunnah za Mtume wetu (صلى الله عليه وآله وسلم) na hadi akapata maadui, kupigwa vita, kutiliwa majungu, kufitinishwa na viongozi na kufungwa jela na kuteswa hadi kufariki kwa ajili ya kuihami hii Dini na mafundisho sahihi ya Qur-aan na Sunnah. Kadhaalika, Shaykh Al-Albaaniy ni katika waliofuata nyayo kwa karibu za Imaam Shaykh al-Islaam Ibn Taymiyyah kwa kufanya Jihaad za kusimamisha mafunzo sahihi ya hii Dini tukufu. (Allaah Awarehemu Wanachuoni hawa rahma kubwa na Awape maghfirah mapana kabisa)

Nataraji kwa Allaah, kazi hii ya historia fupi ya Mwanachuoni huyu, tutakuwa tumesaidia kwa kiasi fulani kuwahamasisha Waislam waweze kufuatilizia kazi zake na kusoma mchango wake mkubwa katika Dini hii na kuweza kunufaika na yote aliyoyaacha Mwanachuoni huyo kutokana na maandishi yake na kutokana na wanafunzi wake wakubwa aliowaacha nyuma yake.

Jina Lake Na Familia Yake

Jina Lake: Muhammad Naaswirud-Diyn bin Nuuh An-Najaatiy

Nasaba Yake: Al-Albaaniy (Kajulikana kwa jina la Al-Albaaniy kwa sababu asili yake ni mtu wa Albania)

Kun-yah Yake: Abu 'Abdir-Rahmaan (Baba ya 'Abdur-Rahmaan')

Wake Zake: Alia wake wanne; watatu wa mwanzo walimzalia watoto, na wa nne 'Ummu Al-Fadhwl' hakujaaliwa kuzaa, na ndiye aliyeishi naye hadi alipofariki dunia.

Watoto Wake: Aliruzukiwa watoto 13; 7 wa kiume na 6 wa kike. Wa kiume ni: 'Abdur-Rahmaan, 'Abdul-Latwiyf, 'Abdur-Razzaaq, 'Abdul-Muswawwir, 'Abdul-Muhaymin, Muhammad na 'Abdul-A'ala. Wa kike ni: Aniyah, Aasiyah, Salaamah, Hassaanah, Sakiynah na HibatuLlaah.

Kumbukumbu Za Ajabu

Mwanachuoni Shaykh Muhammad Naaswirud-Diyn bin Nuuh An-Najaatiy Al-Albaaniy ni mmoja kati ya Ma'ulamaa wakubwa wa Kiislam katika zama hizi. Anahesabika kuwa ni Mwanachuoni wa Hadiyth maarufu kabisa katika fani ya elimu ya *Jarh na Ta'adiy*.⁷

Shaykh Al-Albaaniy vilevile ni hoja katika elimu ya *Mustwalahul-Hadiyth*.⁸ Na Wanachuoni wamemsifu na kuelezea kwamba kwa elimu yake hiyo, karejesha kumbukumbu za zama za kina Imaam Ibn Hajar Al-'Asqalaaniy, Ibn Kathiyr na Wanachuoni wengine wakubwa wa fani hiyo.

Alikuwa na kumbukumbuku ya hali ya juu katika kuhifadhi vitu kichwani na mengine mengi. Kumbukumbu inayotukumbusha wema waliotangulia kama kina Ibn 'Abbaas, Abu Hurayrah (رضي الله عنهم) na waliofuatia kama Imaam Al-Bukhaariy, Imaam Ash-Shaafi'y, Shaykhul-Islaam Ibn Taymiyah, Imaam Ibn Kathiyr, Imaam An-Nawawy na wengine (رحمهم الله).

Kuzaliwa Na Kukua Kwake

Alizaliwa mwaka 1332H – 1914M katika mji wa Ashkoderu ambao kwa wakati huo ulikuwa mji mkuu wa Albania huko Ulaya Mashariki na ukoo wake ulikuwa maskini. Baba yake aliyetitwa Shaykh Nuuh An-Najaatiy alihitimu katika chuo cha Shari'ah huko Istanbul, Uturuki, na

⁷ Ni fani ya Hadiyth inayohusiana na uaminifu wa wasimulizi wa Hadiyth na inakusanya habari zao zinazothibitisha uaminifu au udhaifu wa hao wasimulizi.

⁸ Sayansi ya Hadiyth

kurejea kwao akiwa Mwanachuoni. Lakini baada ya mfalme Ahmad Zogo kutwaa madaraka ya nchi na kuendesha utawala wa nchi hiyo kikomunisti ikabidi baba yake (Shaykh Al-Albaaniy) ahamie Damascus, Syria. Wakati huo Shaykh Al-Albaaniy alikuwa na umri wa miaka tisa.

Imaam Muhammad Naaswirud-Diyn Al-Albaaniy alianza masomo yake ya awali katika madrasah ya Al-Is'aaf Al-Khayriyah hapo Damascus na kuendelea hadi alipomaliza na kuwa msimamizi wa chuo hicho hadi yalipoanza mapinduzi dhidi ya Ufaransa nchini humo. Madrasah hiyo ikakumbwa na maafa ya moto yaliyosababishwa na vurugu na machafuko katika vita hivyo. Baba yake akaamua kumuachisha masomo na akaanza kumsomesha yeye mwenyewe. Alimwekea ratiba kali ya masomo ambayo ni; Qur-aan, Tajwiyd, Swarf, Fiqh (ya Kihanafi, yaliyokuwa madhehebu ya baba yake aliyekuwa Mwanachuoni mkubwa wa madhehebu hayo). Shaykh Al-Albaaniy alijifunza pia masomo mbalimbali ya Dini na lugha kutoka kwa Wanachuoni wakubwa na Mashaykh waliokuwa marafiki wa baba yake kama vile Shaykh Sa'iyd Al-Burhaaniy ambaye alimsomesha masomo ya balaaghah na lugha.

Kujifunza Kwake Elimu Ya Hadiyth

Alitunukiwa shahada ya juu ya elimu ya Hadiyth kutoka kwa Shaykh Raaghib At-Twabbaakh, Mwanachuoni mkubwa wa Halab katika wakati huo. Hapo ni wakati alipokutanishwa naye kupitia Shaykh Muhammad Al-Mubaarak ambaye alimjulisha Shaykh At-Twabbaakh umahiri wa kijana huyo (Al-Albaaniy) katika elimu ya Hadiyth. Baada ya Shaykh At-Twabbaakh kumjaribu na kuthibitisha hilo mwenyewe, akamtunuku shahada (*Ijaazah*). Shahada hiyo si pekee, bali pia alipata kwa Wanachuoni wengine wakubwa wa Hadiyth kama Shaykh

Bahjatul Baytwaar (ambaye isnaad yake inafika hadi kwa Imaam Ahmad bin Hanbal).⁹

Aliingia kwenye fani ya Hadiyth akiwa na umri wa miaka ishirini. Aliathirika sana na tafiti mbalimbali za Muhammad Rashid Ridhwa, Mwanachuoni wa Misr wakati huo. Tafiti hizo zilikuwa katika jarida la *Al-Mannaar*. Anasema Imaam Al-Albaaniy: “Nilichokimulika mwanzo miongoni mwa vitabu, ni vile vya visa vya lugha ya kiarabu, kama vile; *Adhw-Dhwaahir*, *‘Antarah*, *Maalik as-Sayf* na vinginevyo kama hivyo. Kisha nikazama katika vitabu vya visa vya kijasusi vilivyotarjumiwa katika lugha ya Kiarabu. Siku moja nikapita katika vibanda vya kuuza vitabu na macho yangu yakaangaza kwenye jarida moja liitwalo *Al-Mannaar* na katika kupekuapekua ndani yake nikakutana na makala ya kitafiti ya Rashid Ridhwa akikielezea kitabu cha *‘Thyaa ‘Uluum ad-Diyn’* cha Abu Haamid al-Ghazaaliy, akitaja mazuri yaliyomo ndani ya kitabu hicho na kasoro zake. Kwa mara ya kwanza nikakutana na aina kama hii ya uchambuzi wa kielimu. Nilivutika sana na uchambuzi sampuli hiyo na ukanifanya nisome toleo zima la makala hiyo. Kisha nikawa nafuatilizia maudhui za uchambuzi wa Hadiyth wa Mwanachuoni Al-Haafidh Al-‘Iraqiy alioufanya kwa Hadiyth zilizomo ndani ya kitabu *‘Thyaa ‘Uluum ad-Diyn’*. Sikutosheka hadi ikabidi nimuombe muuza duka aniazime jarida hilo kwa kuwa sikuwa na uwezo wa fedha wa kulinunua!

Hapo ndipo ilipoanza safari ndefu ya kusoma vitabu mbalimbali. Nikatoa nakala ya maudhui hiyo iliyofanyiwa uchambuzi wa kina katika jarida hilo”

Shaykh Al-Albaaniy alijifunza pia kwa baba yake elimu ya kutengeneza saa hadi akawa fundi mzuri maarufu kwa kazi hiyo. Ikawa ndiyo kazi iliyompatia rizki yake. Alikuwa fundi na hapo hapo mtafutaji elimu. Hali hiyo ikaendelea hivyo hadi alipoamua kutenga siku mbili tu za kufanya kazi ya kutengeneza saa, na siku zote zilizobaki zikawa ni za kutafuta elimu. Elimu hiyo alikuwa akiichukulia katika maktaba kubwa ya mji huo wa Damascus iliyoitwa *Adhw-Dhwaahiriyah* ambapo alikuwa akitumia siku nzima kusoma na kutafiti. Alishughulishwa mno na

⁹ *Hayaatul Al-Albaaniy*, Muhammad Ash-Shaybaaniy. Al-Albaaniy mwenyewe anayaeleza hayo pia kwenye vitabu vyake *‘Mukhtaswar Al-‘Uluww’* na *‘Tahdhiyru-Saaqid’*.

kusoma hadi akawa anasahau hata kula. Kilichokuwa kinakatisha utafiti na masomo yake ni vipindi vya Swalah tu. Mwishowe, wahusika wa maktaba hiyo wakamuamini na kuamua kumpa funguo zake awe anatumia maktaba wakati wa ziada, na akawa daima ni mtu wa mwisho kutoka na kufunga mwenyewe.

Hadiyith za Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) zilikuwa zina athari kubwa sana katika maisha ya Shaykh kielimu na kiutendaji. Zikamuelekeza katika *Manhaj* (Njia, mwenendo) Sahihi; ambao ni kuchukua kutoka kwa Allaah (Qur-aan) na Mtume Wake (Sunnah) tu. Akipata usaidizi wa ufahamu wa vyanzo hivyo viwili vikuu kutoka kwa Maimaam Wanachuoni katika wema waliotangulia (*as-Salafu as-Swaalih*) bila kuwa na *ta'aswub* (kasumba) ya kumshabikia yeyote miongoni mwao au kumponda yeyote, bali msimamo wake ulikuwa ni kuchukua haki popote ipatikanapo na kutoka kwa yeyote.

Kwa sababu hiyo, aliyaacha na kuyaweka pembeni madhehebu ya Kihanafi aliyokulia nayo na aliyosomeshwa na baba yake. Baba yake (رحمه الله), alikuwa akivutana naye sana juu ya masuala hayo ya kimadhehebu, kwani baba yake alikuwa ameshikilia kwa nguvu sana msimamo wa Kihanafi na hataki kusikia mingine hata iliyokuwa sahihi katika masuala mengine. Shaykh alijaribu sana kumfahamisha baba yake kuwa anapaswa kufanyia kazi Hadiyith za Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) endapo itathibiti usahihi wake, na kuacha ya wengine wote kama hayawafikiani na maneno ya Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم).

Wanafunzi Wake Maarufu

Wanafunzi wake ni wengi sana na walio maarufu katika Mashaykh ni hawa ambao baadhi yao wako hai hadi leo:

Shaykh Muqbil bin Haadiy Al-Waadi'iy (Yemen)

Dkt. 'Umar Sulaymaan Al-Ashqar (Jordan)

Shaykh Saalim Al-Hilaaliy (Palestina)

Shaykh Hamdiy 'Abdul-Majiyd

Shaykh Muhammad 'Iyd 'Abbaasy

Shaykh 'Aliy Hasan

Shaykh Muhammad Ibraahiym Shaqrah (Jordan)

Shaykh 'Aliy Khushshaan

Shaykh Muhammad Jamiyl Zaynuu (Saudi Arabia)

Shaykh 'Abdur-Rahmaan 'Abdus-Swamad

Vitabu Vyake

Maktaba za Kiislam zimeneemeka kwa vitabu vingi vya Shaykh hususan vile vikubwa vyenye mijalada mingi vya '*Silsilatul Ahaadiyith Asw-Swahiyhah*' na '*Silsilatul Ahaadiyith adhw-Dhwa'iyfah wal-Mawdhuw'ah*' na kitabu chake cha Swalah kiitwacho '*Swiftatus Swalaatin Nabbiy*'¹⁰ ambacho kimepokelewa kwa nguvu sana na wasomaji pande zote za ulimwengu, haswa vijana. Ni mojawapo ya vitabu vizuri na muhimu sana katika mafunzo ya Swalah kama ilivyoswaliwa na Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم).

¹⁰ Kitabu hiki kimeshatafsiriwa na mwandishi kwa lugha ya Kiswahili na kinapatikana maeneo mbalimbali kwa jina "Sifa Ya Swalah Ya Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم)". Kitabu hiki kilichapishwa na kinaendelea kuchapishwa kwa malengo ya kutawanywa bure, hivyo msomaji, jitahidi upate nuskha yako ya bure.

Kadhaalika, Shaykh ana vitabu maarufu sana vya Hadiyith vyenye kuvifanyia sharh, tahkiki, na hata kubainisha yale ya sahihi na ya dhaifu ndani ya vitabu hivyo, kama alivyofanya kwenye vitabu *Sunan At-Tirmidhy, Sunan Ibn Maajah, Sunan Abi Daawuud* n.k. Vilevile ana mijalada mingi ya vitabu kama tutakavyoona hapo chini kwenye orodha fupi. Vilevile ameweza kutoa vitabu vya kufafanua na kusahihisha vitabu maarufu vya Wanachuoni wakubwa wa karibuni kama vitabu '*Tamaamul-Minnah Fiyt-Ta'aliyq 'Alaa Fiqhis-Sunnah'* kilichokuwa ni masahihisho ya Hadiyith zisizo sahihi katika kitabu cha Shaykh Sayyid Saabiq kitwacho '*Fiqhus-Sunnah'*, na ana kitabu cha '*Ghaayatul-Maraam Fiy Takhriyj Ahaadiyith Al-Halaal wal Haraam'* ambacho ni usahihisho wa Hadiyith zilizomo katika kitabu cha Dr. Yuusuf Al-Qaraadhwaawiy kiitwacho '*Al-Halaal Wal Haraam Fiy Islaam'*.

Kazi zake za uandishi kuhusu masuala ya Hadiyith zinazidi zaidi ya mia.

Baadhi Ya Vitabu Vyake Vilivyoenea Sana

- 1- *Silsilatul Ahaadiyith Asw-Swahiyhah (Mijalada 1-11)*
- 2- *Silsilatul Ahaadiyith Adhw-Dhwa'iyfah wal Maawdhwuw'ah (Mijalada 1-14)*
- 3- *Al-Irwaa Al-Ghaliyl (Mijadala 1-9)*
- 4- *At-Targhiyb wa At-Tarhiyb (Mijalada 1-4)*
- 5- *Swahiyh wa Dhwa'iyf Sunan Abi Daawuud (Mijalada 1-4)*
- 6- *Swahiyh wa Dhwa'iyf Sunan At-Tirmidhiy (Mijalada 1-4)*
- 7- *Swahiyh wa Dhwa'iyf Sunan Ibn Maajah (Mijalada 1-4)*
- 8- *Mukhtaswar Swahiyh Al-Bukhaariy*
- 9- *Mukhtaswar Swahiyh Muslim*
- 10- *Sharhu Al-'Aqiydah Atw-Twahaawiyah*

- 11- *Ahkaam Al-Janaaiz*
- 12- *At-Tawaswul: Anwa'uhu wa Ahkaamuhu*
- 13- *Kitaabu As-Sunnah*
- 14- *Swalaatu At-Taarawiyh (Qiyaamu Ramadhwaan)*
- 15- *Tamaamul-Minnah Fiyt-Ta'aliyq 'Alaa Fiqhis-Sunnah*
- 16- *Ghaayatul-Maraam Fiy Takhriyj Ahaadiyth Al-Halaal wal-Haraam*
- 17- *Adaabu Az-Zafaaf*¹¹
- 18- *Swifatu Asw-Swalaatin-Nabiy*¹²

Kueneza Kwake Elimu

Baada ya Al-Imaam, Al-Muhadith, Shaykh Abu 'Abdir-Rahmaan Muhammad Naaswirud-Diyn Al-Albaaniy kupata elimu yake akaanza kuwasiliana na watu kwa ajili ya kueneza Da'awah. Alibeba bendera ya Tawhiyd na Sunnah, na akatembelea Mashaykh wengi wa Damascus na kubadilishana nao mawazo na kujadili masuala mbalimbali ya kielimu haswa katika nyanja za Tawhiyd, pia masuala ya kufuata madhehebu kibubusa (bila dalili), masuala ya bid'ah katika Dini na mengine mengi ambayo ni matatizo katika jamii ya Kiislam popote ulimwenguni.

Hali hiyo ya kusimamia haki na kupambana na batili ilimjengea Shaykh heshima kubwa na wafuasi wengi ingawa pia hawakukosekana

¹¹ Kitabu hiki kilishatafsiriwa na mwandishi na kinapatikana kwa jina "Adabu Za Ndoa Katika Sunnah Iliyotwaharika." Chapa za mwanzo kimetawanywa bure na shukurani zote ni Zake Allaah.

¹² Kitabu hiki kimeshatafsiriwa na mwandishi kwa jina "Sifa Ya Swalah Ya Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم)" na chapa za mwanzo vimetawanywa bure na himidi zote Anastahiki Allaah Aliyetukuka.

Kilipoanzishwa chuo kikuu cha Madiynah huko Saudi Arabia, Mwanachuoni mkubwa huko, Shaykh Muhammad Ibraahiym Aalu Shaykh aliyekuwa Rais wa baraza la Ma'ulamaa na mkuu wa chuo hicho, alimchagua Shaykh Al-Albaaniy kuwa mwalimu wa elimu ya Hadiyth na vigawanyo vyake.

Miongoni mwa athari zake Shaykh Al-Albaaniy, aliweka msingi na kanuni ya fani ya somo la elimu ya *'Isnaad'* na akawa ndiye wa kwanza kabisa kufanya hivyo katika vyuo vyote vya Kiislam. Chuo cha Madiynah kikawa ni kinara cha vyuo vingine kwa hilo. Hakika ikhlaasw yake ndiyo iliacha athari kubwa duniani na kumjengea umashuhuri mkubwa na heshima kwa wengi. Hata hivyo, ikhlaasw yake hiyo ilimsababishia uadui kutoka kwa wale waalimu waliotawaliwa na ubinafsi na hivyo kumfanyia hila mbalimbali na majungu kwa wakuu wa chuo hadi ikafikia chuo kutumbukia katika mtego wa wenye husda na kuamua kumsimamisha Shaykh kwa madai kuwa anahamasisha vijana kutumia 'mkono' katika kuondosha munkar katika jamii. Kuna tukio la baadhi ya wanafunzi wake kwenda kuvunja na kuchoma moto maduka yanayouza video za sinema za makafiri zisizo na maadili na kanda za miziki katika mji mtakatifu wa Madiynah.

Tukio hilo lilifanywa na wanafunzi kwa hamasa za kupenda haki pamoja na kuwa Shaykh hakuwatuma kufanya hivyo. Vijana hao - kama alivyo Muislam yeyote mwenye wivu na Dini yake na pia ardhi hiyo takatifu - hawakupenda kuona ardhi yao ikiwa imejaa uchafu na athari za kikafiri.

Uongozi wa chuo ulimlazimisha Shaykh kulaani kitendo hicho, lakini Shaykh hakutoa kauli yoyote juu ya tukio hilo na hivyo kusababisha uongozi kumnyang'anya wadhifa aliokuwa nao na kumfukuza.

Hata hivyo, baada ya miaka kadhaa wakamuomba arejee nchini Saudia na kufundisha tena, na Shaykh bila kuwa na kinyongo kwa dhulma aliyofanyiwa awali, aliitikia wito huo na kurejea na kufanya kazi yake kwa Ikhlaasw kubwa. Haukupita muda akasimamishwa tena!

Pamoja na matukio hayo, inatubainikia wazi kuwa Shaykh hakuwa kama waalimu wanaosomesha kwa ajili ya ajira tu. Yeye alisomesha na kuhakikisha yanafanyiwa kazi yale anayosomesha, ndio maana elimu yake ikawa na taathira kubwa kwa wanafunzi wa chuo hicho na hata ulimwengu mzima hivi leo. Vilevile, kama tutakavyoona mwisho wa Historia yake, ni kwamba, Shaykh hakuweka kinyongo kwa yote aliyotendewa na uongozi na baadhi ya wenye fitna wasiopenda haki na mabadiliko, bali aliacha wasia wa kuhamishwa maktaba yake yote kubwa yenye vitabu vingi na tafiti mbalimbali, kupelekwa katika chuo cha Madiynah kuwafaa wanafunzi na watafutao elimu. Alikuwa na ikhlaasw isiyoyana mfano.

Safari Zake

Shaykh (رحمه الله) alihama kutoka Damascus, Syria alipokuwa akiishi, na kuelekea 'Ammān, Jordan katika mwezi wa Ramadhān 1400H. Akakaa kwa muda kisha akarejea tena Damascus na kutoka huko akaelekea Beirut, Lebanon, na baada ya muda akahama huko na kuelekea Al-Imaraat Al-'Arabiyah Al-Muttahidah (United Arab Emirates). Huko alikaribishwa kwa heshima kubwa na taadhima na wapenzi wake wa huko ambao ni watu walioshikamana na mwenendo wa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) na Maswahaba (رضي الله عنهم). Wakamkirimu kwa kila hali katika Jumuiya yao ya Daarul-Birr, na

Katika kukaa kwake hapo United Arab Emirates, aliweza kupata fursa ya kusafiri nchi za jirani na kukutana na Mashaykh waliokuwa Qatar na kubadilishana mawazo na kujadili masuala mbalimbali ya Dini.

Akarejea tena Damascus na ziara yake ya mwisho nchini United Arab Emirates ilikuwa mwaka 1989M ambako alikwenda kukaa nje ya mji kwenye Jumuiya ya Daarul-Birr kwenye shamba la kiongozi wa Jumuiya hiyo na kufanya darsa zake mbalimbali katika Msikiti uliokuwepo hapo ambao baadaye ulipewa jina la Shaykh kwa kumbukumbu za ziara zake za kielimu hapo, na pia kuenzi mchango wake na elimu yake kubwa.

Mnamo mwaka 1419H, mwaka mmoja kabla ya kifo chake, Waislam duniani walifarijika kuona Shaykh akitambuliwa kimataifa kwa kupewa tuzo kubwa ya kielimu na mchango katika Dini, itambulikanayo kama, 'Tuzo ya Mfalme Fayswal ya Kimataifa'. Ambayo hutolewa kila mwaka katika mchango wa nyanja mbalimbali za jamii, na kwa upande wa Dini hutolewa kwa Mwanachuoni mkubwa katika Ummah wa Kiislam katika elimu maalum ya Dini. Mwaka huo Ash-Shaykh, Al-Imaam, Al-Muhadith, Al-'Alaamah Al-Albaaniy (رحمه الله) alitunukiwa tuzo hiyo kwa mchango wake mkubwa wa elimu ya Hadiyath na vigawanyo vyake.

Tuzo hiyo kubwa ya kimataifa haikuwashangaza Wanachuoni wengi kupewa Shaykh Al-Albaaniy, bali kilichowashangaza ni kuchelewa Shaykh kutambulika na kupewa tuzo kama hiyo muda mrefu nyuma. Hayo ni kutokana na jinsi walivyokuwa wakiitambua elimu yake kwa muda mrefu.

Hiyo itakumbukwa na wengi kuwa ilikuwa ni hadhi kubwa ya heshima ya kuukubali mchango wake wa Dini hii aliyopewa na nchi ya Saudi Arabia pamoja na kwamba walimfukuza mara mbili kutokana na msimamo wake thabiti usioyumba wa kusimamia Al-Kitaab (Qur-aan)

na As-Sunnah pamoja na misimamo yake mingine ya kielimu iliyokuwa ikipingana na Mashaykh wa Saudia. Alikuwa anajali zaidi kumridhisha Allaah tu Pekee. Pamoja na hivyo, Mashaykh wa Saudia walikuwa wakimheshimu sana na kumpenda kama tutakavyoona mwisho katika kauli zao kumhusu Shaykh.

Upinzani

Kama tulivyoona nyuma, kuwa Shaykh alikuwa akipata upinzani mbalimbali tangu alipokuwa kwenye nchi yake hadi alipokwenda nje kufundisha na kueneza elimu. Wengi waliokuwa wakimfanyia uadui na fitna kwenye serikali tawala, ni wale waliokuwa wanatetea mambo yasiyo na dalili wala uthibitisho katika Dini. Wanachuoni walioweka matamano ya nafsi zao mbele na kuendekeza uluwa wa kidunia na kuimarisha bid'ah katika Dini, ndio waliomchukia Shaykh kwa sababu alikuwa mstari wa mbele kupinga maovu hayo na kubaini kwenye vitabu vyake. Watu wa bid'ah na matamano ya nafsi zao, ndio waliokuwa wakimfanyia chuki na majungu hadi akafungwa jela na hata kuchukiwa na wachache wenye kuendekeza batili.

Mmoja katika waliokuwa wakikeshwa kumpiga vita Shaykh, ni kiongozi wa Kisufi aitwaye Hasan bin 'Aliy As-Saqaaf ambaye alikuwa huko Jordan na ndiye katika waliochangia sana kumfanyia Shaykh majungu mengi ambayo hakika hayakusaidia kumuharibia Shaykh zaidi ya kumfanya ajulikane zaidi na watu wapate kuvijua na kuvisoma vitabu vyake vilivyowafanya wamuheshimu badala ya kumchukia!

As-Saqaaf alitunga vitabu kumkosoa Shaykh kwenye masuala ya Hadiyth, na pia baada ya yeye kuona mafanikio makubwa ya kuenea na kununuliwa kwa wingi kitabu cha Shaykh kiitwacho '*Swifatus-Swalaat An-Nabbiy'*, As-Saqaaf akaandika kitabu dhidi ya hicho! Hata hivyo, vitabu vyake vilijibiwa kielimu na wanafunzi wa Shaykh Al-Albaaniy.

Licha ya kumshambulia Shaykh Al-Albaaniy, vilevile kuna mengi aliyoyaandika As-Saaqaaf kwenye vitabu vyake kushambulia baadhi ya Maswahaba (رضي الله عنهم).¹³

Miongoni mwa sifa kubwa za Shaykh Al-Albaaniy zilikuwa ni kukabiliana na wote waliompinga na kujadiliana nao kwa hoja na dalili. Na hivyo ndivyo alivyofanya kwa As-Saaqaaf. Alikwenda nyumbani kwa As-Saaqaaf baada ya kuahidiana kujadili mada kuhusu 'At-Tawasul', na alipofika kwake akakuta kinyume na alivyotarajia kwa kudhani kuwa As-Saaqaaf ni katika 'wajukuu wa Mtume' kama alivyokuwa akijiita, ingawa vitendo alivyovikuta - kama anavyosema mwenyewe - havikuwa kama vya babu yake [yaani Mtume صلى الله عليه] (وآله وسلم), kwani alikuwa na kiburi, ukubwa, ufakhari na kupenda kutukuzwa.

Shaykh Al-Albaaniy alipotaka waanze mjadala uliomleta hapo, As-Saaqaaf akawa anazunguka huku na kule kwa mada zingine bila kuzungumzia walichopanga awali. Shaykh kwa utulivu, alivumilia yote na mwishoni aliondoka bila kufikia alilolifuata. Baada ya hapo, As-Saaqaaf akawa anamtukana Shaykh Al-Albaaniy kwenye kanda, vitabu na majukwaa. Shaykh Al-Albaaniy hakuwahi kumtukana wala kuandika vitabu vya kumtukana kama alivyofanyiwa yeye. Insaafu hiyo na uadilifu mkubwa wa Shaykh ulimzidishia sana wapenzi na kukubalika.

Tukio moja lilinidhirishia utukufu wa hali ya juu sana wa Shaykh Al-'Alaamah, nilipokuwa nasikiliza mawaidha yake, na hususan majibu ya maswali na matukio mbalimbali aliyokuwa akikabiliana nayo nyumbani kwake - nyumba ambayo mlango wake ulikuwa wazi masaa yote kwa wageni - pale alipotembelewa na wawakilishi wa As-Saaqaaf. Wageni hao walijitambulisha kuwa wao ni vijana na wanafunzi wakubwa wa As-Saaqaaf.

¹³ *Daf'u Shubuhaat at-Tashbiyh*, uk. 237.

Shaykh aliwapokea vizuri sana kwa heshima kubwa. Na katika mazungumzo walikuja kwa mijadala mbalimbali kuhusu masuala ya 'Aqiydah na huku wakimtuhumu Shaykh kuwa anamfananisha Allaah na viumbe, na masuala mengine kadhaa. Shaykh kwa upole na bashasha alianza kuwauliza mahali waliposikia hayo na ushahidi wake, wakawa hawana, na akaendelea kujadiliana nao kwa masaa yasiyopungua manne, kwa mjadala mkali wa kielimu bila Shaykh kukasirika wala kuchoka Mwishowe vijana hao waliondoka kwa Shaykh kwa heshima kubwa sana na kumuomba Shaykh aandike kitabu kuhusu 'Aqiydah ili aweke wazi msimamo wake kuhusu sifa za Allaah (سبجانه وتعالى) maana baadhi ya watu wanamtungia uongo na kumtuhumu.¹⁴

Huo ni mfano wa Mwanachuoni wa aina ya nadra sana katika ulimwengu huu.

Vilevile Shaykh Al-Albaaniy aliwahi kujadiliana na mahasimu wake wengine kama kiongozi mwengine mwenye mitazamo ya kisufi wa Syria aitwae Muhammad Sa'iyd Ramadhaan Al-Buutwiyy ambaye alipinga sana mtu kutokuwa na madhehebu na ameandika vitabu vya kushambulia watu wenye kutotaka kujinasibisha na madhehebu maalum. Shaykh Al-Albaaniy alijaribu mara nyingi kumwandikia barua ya kukutana naye na kuyajadili masuala hayo na mengineyo lakini ilichukua muda mrefu hadi Al-Buutwiyy kukubali. Walikutana kwenye mjadala uliodumu masaa matatu na mwisho wa mjadala Al-Buutwiyy alidhihirika kuwa hoja zake zilikuwa dhaidu na akakataa mjadala mwingine alioombwa na Shaykh Al-Albaaniy.¹⁵

Uhusiano Wake Na Wanachuoni

¹⁴ *Bid'atut Ta'aswub al-Madh-habiy*, Shaykh 'Iyd al-'Abbaasiyy. Na pia nakala ya mjadala huo inapatikana kwenye mtandao.

¹⁵ Mjadala huo wa Shaykh Al-Albaaniy na Al-Buutwiyy unapatikana kwenye mtandao.

Imaam Al-Albaaniy alichunga sana heshima na mahusiano bora na Ma'ulamaa wenzake. Mahusiano aliyokuwa akiyajenga kwa misingi ya haki na ukweli. Aliwaheshimu Wanachuoni wenzake na kujifunza mengi kutoka kwao. Hakuwastahi katika haki haswa walipokosea. Alikuwa na njia nzuri za kukosoa na kutoa nasaha kwa wenzake. Alipokuwa anapata kitabu cha Mwanachuoni mwenzake au mlinganiaji au mwandishi wa Kiislam na kukuta ndani kuna makosa ya 'Aqiydah, Hadiyth au Fiqh, alikuwa hachelewi kuwasiliana naye kwa maandishi, kwa simu, au hata kuwafuata japo waliishi mji au nchi za mbali.

Mifano mizuri ya hili, ni barua zake kwa Muhammad Mitwaliy Ash-Sha'arawiy aliyekuwa Misr, Sayyid Saabiq aliyekuwa Misr vilevile, Yuusuf Al-Qaaradhwaawiy (Mmisri) ambaye hivi sasa ni Mufti wa nchi ya Qatar na kiongozi wa 'Umoja wa Ma'ulamaa Duniani'. Pia aliwahi kukutana nao uso kwa uso na kujadiliana nao mas-alah mbalimbali.

Kadhaalika, aliandika vitabu vya kusahihisha Hadiyth zilizomo kwenye vitabu vya hao aliowarekebisha.¹⁶ Pia alikuwa anawasiliana na Mashaykh wakubwa wa Saudia kama Shaykh 'Abdul-'Aziyz bin Baaz (رحمه الله) na kujadili masuala mbalimbali ya ki-Fiqh. Pamoja na kutofautiana kwao hawakugombana wala kupunguza mapenzi baina yao kama tutakavyoona mwisho maoni ya Shaykh 'Abdul-'Aziyz bin Baaz (رحمه الله) na wengineo kuhusu Shaykh Al-Albaaniy.

Fadhila Na Mema Yake

¹⁶ *Tamaamul Minna fiy Takhriyj Ahaadiyth Fiqhis-Sunnah, Ghaayatul Maraam fiy Takhriyj Ahaadiyth al-Halaal wal-Haraam.*

Shaykh Al-Albaaniy (رحمه الله) alikuwa ni mwenye kufuata mwenendo wa wema waliotangulia (*Salafus-Swaalih*), akifuata mwenendo wao na tabia zao, na yakawa macho yake yanafuata kilichosemwa na Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) na Mtume Wake (سبحانه وتعالى).

Alikuwa hastahi katika haki, akiitangaza haki katika vitabu na mihadhara yake. Hii ni sifa ya nadra sana kuipata katika ulimwengu wa leo, ambao wengi hawapendi kusema haki kwa kuchelea kuwaudhi wengine au kupoteza kukubalika. Shaykh alikuwa akijirudi pindi alipokutana na dalili sahihi inayokwenda kinyume na kauli yake, na aliacha kauli yake na kufuata dalili hiyo iliyosihili bila kuangalia imetoka kwa nani. Kuna baadhi ya Hadiyth alizokuwa akiitakidi kuwa sahihi kwa elimu yake, na baadaye zikambainikia au akatanababishwa kuwa si sahihi, akawa anajirudi haraka na kukubali na kuzitaja katika vitabu vyake. Sifa hiyo pamoja na uzuri wake, lakini kuna waliokuwa na chuki wakatumia kumtilia kasoro na kudai kuwa ‘anajigongagonga’, na hadi wakaandika vitabu kumkosa kwa sababu hiyo!!

Sifa hiyo ndiyo waliyokuwa nayo Maimaam wanne wa Sunnah, ambao misimamo yao ni pale ilipothibiti dalili sahihi kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم).

Walikuwa na kauli nyingi kuhusu hayo, hapa nitaorodhesha chache:

Imaam Abu Haniyfah (رحمه الله)

“Ikiwa Hadiyth imeonekana kuwa ni sahihi, basi hiyo ndiyo madhehebu yangu.” “Hairuhusiwi kwa mtu yeyote kukubali rai zetu ikiwa hawajui wamezipata kutoka wapi”.¹⁷

¹⁷ Ibnul-'Aabidiyn katika *al-Haashiyah* 1/63, na katika inshaa yake *Rasm al-Mufti* 1/4 kutoka Mkusanyiko wa Insha za Ibnul-'Aabidiyn. Shaykh Swaalih Al-Fulaaniy

Katika riwaya nyingine: “Imekatazwa mtu ambaye hajui dalili zangu kutoa hukmu kutokana na maneno yangu”

Katika riwaya nyingine imeongezwa: “...Kwani sisi ni wanaadamu, tunasema jambo siku moja na kulirudisha siku ya pili yake.”

Imaam Maalik (رحمه الله)

“Hakika mimi ni mwanaadamu: Ninafanya makosa (mara nyingine) na ninakuwa sahihi (mara nyingine). Kwa hiyo, tazameni rai zangu; zote zinazokubaliana na Kitabu (Qur-aan) na Sunnah, zikubalini; na zote zisizokubaliana na Kitabu (Qur-aan) na Sunnah, basi zipuuzeni.”¹⁸

Imaam Ash-Shaafi'iy (رحمه الله)

“Ukiona katika maandishi yangu jambo ambalo ni tofauti na Sunnah ya Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم), basi zungumza kwa kurejea Sunnah ya Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) na acha niliyoyasema mimi”

Katika usimulizi mwingine: “...basi ifuate (Sunnah) na usitazame tena pembeni kufuata usemi wa mwengine yeyote”¹⁹

katika *al-Iyqaadhw al-Himaam*, uk. 62. Na hii imeelezwa na Imaam Ibn 'Abdil-Barr kutoka Abu Haniyfa na kutoka kwa Maimaam wengine.”

¹⁸ Ibn 'Abdil-Barr katika *Jaami'ul Bayaan Al-'Ilm*, 2/32, ibn Hazm akinukuu kutoka kwake katika *Usuul-Al-Ahkaam* 6/149, na hali kadhaalika Al-Fulaaniy, uk. 72.

¹⁹ Harawiy katika *Dhamm Al-Kalaam* 3/47/1, Al-Khatwiyb katika *Al-Ihtijaaj bi Ash-Shaafi'iy* 8/2, Ibn 'Asaakir 15/9/10, An-Nawawiy katika *Al-Majmuu'* 1/63, Ibn al-

Na akasema:

“Hadiyth ikipatikana kuwa ni Swahiyh, basi hiyo ndio madhehebu yangu.”²⁰

Imaam Ahmad bin Hanbal (رحمه الله)

Msifuate rai yangu, wala msifuate rai ya Maalik, au Ash-Shaafi'iy au ya Awzaa'iy, wala Thawriy, lakini chukueni kutoka walikotoa,”²¹

Sifa hiyo waliyokuwa nayo hao Maimaam wanne wakubwa na yeye kuifuata ndiyo iliyomfanya Shaykh kupendwa na kupata wafuasi wengi kila pande ulimwenguni. Na ndiyo vilevile iliyomfanya kupata wenye kumchukia.

Shaykh ameacha athari kubwa katika elimu ya Hadiyth hadi imefikia sasa Wanachuoni wengi wanapotaja Hadiyth basi hawaachi kutaja usahihi au udhaifu wa Hadiyth hiyo kwa mujibu wa uchambuzi wake.

Alikuwa haachi kufunga Swawm za Sunnah haswa za Jumatatu na Alkhamiys katika maisha yake ila tu alipokuwa safarini.²²

Qayyim 2/361, na Al-Fulaaniy, uk. 100, usimulizi wa pili ni kutoka *Hilyah Al-Awliyaa* ya Abu Nu'aym.

²⁰ An-Nawawiy katika *Al-Majmuu'* 1/63, Ash-Sha'raaniy 1/57, akitoa chanzo chake kama Al-Haakim na Al-Bayhaqiy na Al-Fulaaniy, uk. 107.

²¹ Al-Fulaaniy, uk. 113, na Ibn Al-Qayyim katika *I'laam Al-Muwaqqi'iyin*.

Nyumba yake ilikuwa 'ingia toka' ya watu wa kila aina waliokuwa wakija kwake kutafuta elimu, kuuliza masuala ya Dini, kutatuliwa masuala ya kijamii, kifamilia, na hata kuhitaji misaada mbalimbali pamoja na kuwa hali ya Shaykh ilikuwa ya wastani. Hata hivyo, alikuwa haachi kuwasaidia waliomfuata kwa shida.

Katika baadhi ya nyakati Shaykh alikuwa akitaja jinsi alivyokuwa siku za nyuma akiokota makaratasi njiani au kadi zilizotupwa au kupekua kwenye sehemu zilitupwa karatasi ambazo alikuwa akizitumia kuandikia Hadiyth. Yote ni kutokana na hali ya umaskini na shida kwa kutokuwa na uwezo wa kununua madaftari ya kuandikia.

Alikuwa akichunga sana wakati. Hakuwa akiacha sekunde ya maisha yake ipite bila kuifanyia kazi na kuchuma ujira kutoka kwa Allaah (سبحانه وتعالى). Alikuwa mwingi wa kufanya dhikr, kufundisha, na kujifunza kutoka kwa wengine.

Sifa yake ya kujifunza ilikuwa haina mithali! Alikuwa akitumia zaidi ya masaa kumi na nane (18) kwa siku katika maktaba yake kupitia na kufanya rejea mbalimbali, kutafiti na kuandika! Muda aliokuwa akikatisha masomo na utafiti wake ulikuwa ni wa kuswali na kula kidogo.

Waliobahatika kukutana na Shaykh wanashuhudia utaratibu wake, heshima yake na ucha Mungu wake wa hali ya juu. Alikuwa haachi fursa bila kumfundisha mtu kitu kipya au kumkosoa kwa utulivu na busara. Siku moja alipokuwa Hospitali amelazwa, Daktari aliyekuwa amenyoa ndevu zake zote aliingia na kumpa dawa na baada ya kumaliza akiwa anaondoka, akamuomba Shaykh amuombee Du'aa, Shaykh akaomba na kusema "Namuomba Allaah Akupendezeshe kwa kile kinachompendeza mwanaume."

²² Samiyr bin Amiyn Az-Zuhayriy, *Muhadith Al-'Aswr*, uk. 39.

[Makusudio ya Shaykh hapa yalikuwa ni kuwa yule Daktari apendezeshwe kwa kuongozwa kuweka ndevu, kwani ni jambo lililosisitizwa sana na Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم)].²³

Kila Alfajiri Shaykh alikuwa akipita na gari lake kwenye nyumba za wanafunzi wake kuwaamsha kwa ajili ya Swalah ya Alfajiri.²⁴

Kwa kuchelea kwake 'riyaa', wakati mmoja alijiwa na ujumbe wa watu kutoka Bangladesh na kumwalika akafanye ziara ya wiki moja kutoa mihadhara kwa watu waliokuwa wakimsubiri ambao idadi yao ilikuwa haipungui mamilioni! Shaykh alishtushwa sana na akakataa kabisa. Ujumbe ule ukamuomba akubali japo siku tatu. Shaykh akakataa! Wakamuomba siku moja, akataa! Mwisho wakamwambia basi kwa mhadhara mmoja tu kisha watampakia kwenye ndege arudi siku hiyo hiyo. Shaykh hakukubali na ujumbe ukaondoka ukiwa na huzuni kubwa. Alipoulizwa Shaykh sababu iliyomfanya akatae fursa hiyo kubwa ya kutoa elimu kwa watu wengi kiasi hicho, Shaykh akajibu: "Watu wote hao wananisubiri! Je, nitasalimika na riyaa katika hali kama hiyo?"

Alikuwa akiendesha baiskeli yake kutoka Damascus kuwafuata Waislam kwenye vitongoji vingine, kwa masafa ya kilomita 45 kwenda kutoa elimu.

Alikuwa akiingia Msikitini siku ya Ijumaa, akiswali Raka'ah mbili mbili za *Naafilah* (Sunnah) na akiendelea hadi Khatwiyb alipopanda minbar kuanza kutoa Khutbah.²⁵

²³ Samiyr bin Amiyn Az-Zuhayriy, *Muhadith Al-'Aswr*, uk. 30.

²⁴ Shaykh Husayn Al-'Awaashah, *Swafahaat Baydhwaa Min Hayaat Shaykhina Al-Albaaniy*, uk. 38.

²⁵ Samiyr bin Amiyn Az-Zuhayriy, *Muhadith Al-'Aswr*, uk. 39.

Elimu Yake Na Athari Yake Kwa Watu

Shaykh alikuwa katika daraja ya *Al-Haafidh* (Mwanachuoni wa Hadiyth aliyehifadhi Hadiyth laki moja (100,000) pamoja na mnyororo wa wapokezi wake na 'mutuun' zake (maneno ya kila Hadiyth). Hayo yanaelezwa na Shaykh 'Ashiysh aliyemuuliza suala hilo na Shaykh akakataa kumjibu kwa unyenyekevu na kutotaka kujifakharisha, alichojibu baada ya kukazaniwa sana swali hilo, alijibu kwa Aayah hii: **{{Na neema yoyote mliyonayo inatoka kwa Allaah}}** An-Nahl: 56.²⁶

Katika wasia wake Shaykh alitoa hadiya maktaba yake ya vitabu na kazi zake za uandishi kukitunuku Chuo Kikuu Cha Madiynah kama alivyosema katika wasia wake: "Nimeiachia maktaba yangu - vyote vilivyomo, vikiwa ni vilivyochapishwa tayari, au nakala, au kazi nilizoziandaa kuchapishwa; kwa maandishi ya mkono wangu, au ya mwengine aliyeniandikia - kwa kuipa maktaba ya *Jaami'atul-Islaamiyah* (Chuo Cha Kiislam) kilichopo katika mji wa Madiynah. Kwa sababu ni kumbukumbu nzuri kwa chuo hicho wakati nilipokuwa huko nikifundisha, kwa kulingania kwake kwa msingi wa Kitaab (Qur-aan) na Sunnah kwa kufuata mwenendo (*Manhaj*) wa wema waliotangulia (*Salafus-Swaalih*)".²⁷

Alikuwa hapendi kuitwa Mwanachuoni na mara nyingi akijiita '*Twaalibul-'Ilm*', Mtafutaji elimu.

Siku moja mwanamke kutoka Algeria alimpigia simu na kumwelezea kuwa mwenzake (dada wa Kiislam) kamuota kwenye ndoto, akiwa na

²⁶ Shaykh Husayn Al-'Awaashah, *Swafahaat Baydhwaa Min Hayaati Shaykhina Al-Albaaniy*, uk. 40.

²⁷ Samiyar bin Amiyn Az-Zuhayriy, *Muhadith Al-'Aswr*, uk. 78.

Shaykh alipambana na kila aina ya upotofu na mojawapo ni mtu aliyedai kapewa utume. Kwa utulivu bila hasira wala kutaka kumlaani na kumshambulia pamoja na kuwa ni dai la ukafiri ulio wazi. Shaykh alimsikiliza kwa makini na kumuuliza maswali na kuzikatakata hoja zake hadi mwisho baada ya masaa, yule mtu akaomba Tawbah kwa Allaah (سبحانه وتعالى).²⁹

Watu waliokuwa wakimtukana walikwenda kwake na huku wakimtuhumu kuwa ni kafiri, na bila kukasirika na kugombana nao akajadiliana kwa upole na mapenzi na ilipofika wakati wa Swalah wakakataa kuswalishwa naye. Hakukasirika bali aliomba mmoja wao aswalishe na yeye kumfuata! Baada ya Swalah hiyo wakaendelea na mjadala na ilipofika Swalah nyingine, wao wenyewe wakamuomba Shaykh awaswalishe!! Akawa kwao si kafiri tena, bali Mwanachuoni mwenye kuheshimiwa kabisa.

Alikuwa mtu wa kawaida sana, mnyenyekevu asiye na makuu na asiyetofautishwa na watu wengine ila kwa vitendo na maongezi yake ya kielimu.

Katika kipindi cha maisha yake, alifanya tafiti nyingi na kuzichambua taqriban silsilah 30,000 za wasimulizi wa Hadiyath (*isnaad*), akiwa ametumia kiasi cha miaka 60 ya umri wake kusoma na kupitia vitabu vya Sunnah na kuwa karibu navyo kwa muda wote huo, na

²⁸ Unaweza kusikiliza mazungumzo hayo kwenye mtandao unaoitwa: “*Indama Bakaa Al-Albaaniy (Rahimahu Allaah) [رحمه الله] عندما بكى الألباني...!*”

²⁹ Unaweza kusikiliza mjadala huo unaoitwa: “*Munaadhwarah Ma’a Rajul-id-Da’aa An-Nubuwwah مناظرة مع رجل ادعى النبوة*”

mawasiliano ya nyanja hiyo, na pia kuwa karibu na Ma'ulamaa wa elimu hiyo.³⁰

Wanachuoni wengi walimuheshimu sana na kumtegemea katika masuala ya uchambuzi na uhakiki wa Hadiyth na wakawa wanamtumia kusahihisha vitabu vyao walivyoandika. Shaykh Muhammad Mustafa 'Azami (Mkuu wa kitengo cha Sayansi ya Hadiyth katika Chuo kikuu cha Makkah) alimchagua Shaykh kupitia vitabu vyake vilivyofika mijalada minne ili ahakikishe usahihi wake na pia kuweka maelezo yake ndani. Huo ilikuwa ni ushahidi kutoka kwa Ma'ulamaa kuiamini elimu yake na ubingwa wake wa Hadiyth. Kama ambavyo Chuo Kikuu Cha Madiynah kilipomchagua yeye kupitia na kuhakiki na kuweka maelezo yake kwenye kitabu maarufu cha Hadiyth kiitwacho '*Mishkaat Al-Maswaabiyh*'.³¹

Aliwaheshimu sana Wanachuoni wenzake na kuwaenzi. Siku moja aliletewa habari za masikitiko makubwa kutoka kwa mwanafunzi wake kifo cha Mwanachuoni mkubwa wa zama hizo, Shaykh 'Abdul-'Aziy bin Baaz (رحمه الله), Shaykh Al-Albaaniy alibubujikwa na machozi na kuomba: ((*Innaa Lillaahi wa innaa ilayhi raaji'uun; Allaahumma Ajurniy fiy muswiibatiny wa Akhlifniy khayram minhaa*))

[Kwake Allaah tumetoka na Kwake ndio tutarejea. Ee Allaah, nilipe kwa msiba wangu huu na nibadilishie bora kuliko hicho (ulichokichukua)] Hii ni Du'aa inayoombwa na yule aliyepewa taarifa ya kifo kama ilivyofundishwa na Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم).³²

³⁰ Abu Hudhayfah: 20 Points Regarding Shaykh al-Albaanee

³¹ Abu Hudhayfah: 20 Points Regarding Shaykh al-Albaanee

³² Swahiyh Muslim, Mjalada 2, uk. 632 (*Mulhaq Al-Aswaalah Fiy Wafaat Mujaddid Al-Qarn Wa Muhadith Al-'Aswr*, 25 Jumaadah Al-Aakhirah 1420, uk. 3.

Kipindi Cha Mwisho Cha Maisha Yake

Shaykh (رحمه الله) hakutulia kutafuta elimu hadi umri wa miaka 86, akisoma, akifundisha, akielimisha, akiandika vitabu, akiandika barua kwa Wanachuoni wenzake kuwapongeza, kuwanasihi, kuwakosoa makosa ya vitabuni mwao au fatwa zao. Hadi umri huo hakuwa akiacha kutafiti masuala ya Hadiyith, akipangua sahihi na dhaifu na za kutungwa, aliweza kugawa vitabu vingi vikubwa vya Hadiyith kama vya Maimaam Abu, Dawuud, Ibn Maajah, At-Tirmidhy, An-Nasaaiy na wengineo, akaweza kuvigawa Sahihi zake na Dhaifu zake na kuwasaidia kuwarahisishia wenye elimu na wanafunzi katika uandishi na tafiti zao.

Shaykh anakumbukwa sana kwa kazi hiyo iliyosaidia Ummah leo hii, na kuuamsha kujua Hadiyith sahihi na dhaifu na pia kuwafanya wengi wawe karibu na kuifuatilia elimu ya Hadiyith na sayansi yake. Aliyafanya yote hayo - kwa sababu moyo wake ulikuwa umefungamana nayo hayo kwa mapenzi ya juu - na hakuacha hadi taqriban miezi miwili ya mwisho ya maisha yake, alipokuwa dhaifu akiugua kitandani. Pamoja na magonjwa mazito yaliyomdhoofisha sana na kutotoka kitandani, hakuacha kusoma wala hakupoteza kumbukumbu zake, akiwa anamjua kila aliyekwenda kumtazama, akimuita kila mmoja kwa jina lake! Hadi Allaah (سبحانه وتعالى) Alipoirejesha roho yake na akamfisha katika nyakati za mwisho za Alasiri, siku ya Jumamosi, tarehe 22 katika mwezi wa Jumaadah Al-Aakhirah, mwaka 1420H sawa na 10-02-1999M huko 'Ammaan, Jordan.

Kifo Chake Na Jinsi Kilivyoathiri Ummah

Alizikwa siku hiyo hiyo aliyofariki, pamoja na kuwa alizikwa usiku, lakini idadi ya watu ilikuwa kubwa kuweza kuzidi maelfu kwa maelfu.

Wanachuoni, watafuta elimu, wanafunzi, na watu wa kawaida wote waliathirika sana na kifo cha Shaykh. Taarifa za kifo chake zilipowafikia Waislam, majonzi yalienea pote na wengi kuhisi kuwa ile elimu na yule 'Mujaddid' (Mkarabati wa Dini) wa zama hayupo nao tena. Mwaka huo ulikuwa ni mwaka wa huzuni, kwa kutanguliwa na kifo cha Mwanachuoni mkubwa wa zama hizo hizo ambaye alikuwa Mufti wa Saudia wa wakati huo, Shaykh Al-'Alaamah 'Abdul-'Aziyz bin 'Abdullaah bin Baaz, na baada yao kufuatiwa na kifo cha Mwanachuoni Shaykh Muhammad bin Swaalih Al-'Uthaymiyn, Mashaykh wengine wakubwa waliofariki katika mwaka huo ni, Shaykh Swaalih bin 'Aliy Ghaswuun, Shaykh 'Aliy Twantwawiy, Dkt. Mustwafaa Az-Zarqaa, Shaykh Mana'a Al-Qahtwaan na Shaykh 'Atwiyah bin Muhammad Saalim (Allaah Awarehemu wote hao na Awaweke katika pepo Yake Tukufu).

Sifa Njema Na Heshima Walizotoa Wanachuoni Kwake

**Sifa Njema Walizotoa Ma'ulamaa Kwa Mujaddid Wa Zama
Hizi Shaykh Muhammad Naaswirud-Diyn Al-Albaaniy
(رحمه الله)**

**Shaykh 'Abdul-'Aziyz Bin Baaz [Aliyekuwa Mufti Wa
Saudi Arabia] (رحمه الله)**

Sikumuona mtaalamu wa Hadiyth za Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) katika enzi yetu ya leo chini ya qubah la mbingu kama Mwanachuoni mkubwa Muhammad Naaswirud-Diyn Al-Albaaniy. Aliulizwa kuhusu Hadiyth ya Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم) isemayo:

“Allaah Hutuma kwa Ummah huu Mwanachuoni katika kila miaka mia mtu wa kupiga msasa mambo ya dini Yake”.³³ Aliulizwa ni nani mpiga msasa wa karne hii? Akajibu: Ninadhani Shaykh Muhammad Naaswirud-Diyn Al-Albaaniy, ndiye mpiga msasa wa zama hizi. Na Allaah Ndiye Mjuzi zaidi.

Mwanachuoni Shaykh Muhammad Ibn Swaalih Al- 'Uthaymiyn (رحمه الله)

Yale niliyoyajua kuhusu Shaykh na ambayo ni kidogo wakati nilipokuwa nakutana naye, ni kuwa yeye ana shime ya hali ya juu ya kutumia Sunnah na kupiga vita bid'ah; sawasawa katika 'Aqiydah au matendo. Ama kwa kusoma kwangu vitabu vyake, hakika nimemjua vyema kwa hayo. Ana elimu kubwa ya Hadiyth kwa upande wa Riwaayah na Diraayah. Allaah Amewanufaisha watu wengi kutokana na yale aliyoyaandika kwa upande wa elimu, mfumo na mwelekeo katika taaluma ya Hadiyth. Hii ni faida kubwa sana kwa Waislam. Himdi ni za Allaah. Ama kwa upande wa uhakiki wake wa kitaaluma katika fani ya Hadiyth, basi hayo hayasemekiki.

³³ Imepokewa na Abu Daawuud, na imeelezwa kuwa ni sahihi na Al-'Iraaqiy na wengineo.

Mwanachuoni Mfasiri Shaykh Muhammad Al-Amiyn Ash-Shanqiytwiy (رحمه الله)

Shaykh 'Abdul-'Aziyz Al-Haddaah anasema:

“Hakika Mwanachuoni mkubwa Ash-Shanqiytwiy anamtukuza Shaykh Al-Albaaniy utukuzo wa kushangaza. Anapomuona anapita nailhali yeye yuko katika darsa yake katika Msikiti wa Madiynah, kisha husimamisha darsa lake, husimama na kumsalimia kwa ajili ya kumuheshimu”.

Shaykh 'Abdul-Muhsin Al-'Abaadiy (حفظه الله)

Bila shaka Shaykh Al-Albaaniy, alikuwa ni katika Ma'ulamaa wa kipekee walioumaliza umri wao katika kuitumikia Sunnah, kuitungia vitabu, kulingania kwa Allaah Mtukufu, kuinusuru 'Aqiydah ya kisalafiya, kuipiga vita bid'ah, na kutetea Sunnah ya Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم). Yeye ni katika Ma'ulamaa wazuri wenye sifa za kipekee. Sifa zake zimeshuhudiwa na watu maalumu na wa kawaida. Hakuna shaka kwamba kumpoteza Mwanachuoni kama huyu, ni katika misiba mikubwa inayowapata Waislamu. Allaah Amlipe kheri nyingi kutokana na juhudi zake kubwa na Amweke katika Pepo Yake pana.

Shaykh 'Abdullah Al-'Ubaylaan (حفظه الله)

Ninajipa pole mwenyewe, na ninawapa pole ndugu zangu Waislamu kote duniani kwa kufariki Imaam Mwanachuoni Mkubwa Mhakiki Mcha Mungu Shaykh Muhammad Naaswirud-Diyn Al-Albaaniy.

Ukweli ni kwamba maneno hayawezi kumzungumzia mtu huyu. Ninachoweza kukisema ni kuwa yeye hakukulia katika mazingira ya kisalafiya, lakini pamoja na hivyo, amekuwa ni katika walinganiaji wakubwa wa Salafiyyah, na kufanya mambo kwa mujibu wa Sunnah, na kutahadharisha mambo ya bid'ah. Hata Shaykh wetu 'Abdullaah Ad-Duwaysh anayezingatiwa kuwa ni katika wahifadhiji wachache sana katika enzi yetu na ambaye alifariki akiwa kijana, alisema: "Tokea karne nyingi, hatukumuona mtu kama Shaykh Naaswir kutokana na mengi aliyoyaandika na kuyaelezea, na uhakiki wake ni mbora kabisa. Baada ya As-Swuyutwy hadi hivi leo, hakuna aliyeifanyia uhakiki taaluma ya Hadiyth kwa kiasi kikubwa na usahihi kama Shaykh Naaswir.

Mufti Wa Zamani Wa Saudia Mwanachuoni Shaykh Muhammad Bin Ibraahiym Aal Shaykh (رحمه الله)

Amesema kuhusu Shaykh Al-Albaaniy (رحمه الله): "Yeye ni mwana Sunnah, mpiganiaji haki, na mwenye kupambana na watu wasiofuata haki".

Mwanachuoni Shaykh Zayd Bin Fayyaadh (رحمه الله)

Hakika Shaykh Muhammad Naaswiru-ud-Diyn Al-Albaaniy ni katika Ma'ulamaa wakubwa waliochomoza katika zama hizi. Alizishughulikia Hadiyth, njia zake, wapokezi wake na kiwango chake cha kuwa ni sahihi au si sahihi. Hii ni kazi kubwa ya kheri iliyochukua muda mrefu na kutolewa juhudi kubwa. Yeye ni kama Ma'ulamaa wengine waliokuwa wakipatia na kukosea. Lakini kubobea kwake katika

taaluma hii tukufu, kumeufanya ubora wake ujulikane, na yeye ashukuriwe.

Mwanachuoni Shaykh Muqbil Al-Waadi'iy (رحمه الله)

Hakika katika taaluma ya Hadiyih, hakuna mtu kama Shaykh Muhammad Naaswirud-Diyn Al-Albaaniy. Na Allaah Amenufaisha kwa elimu yake na vitabu vyake mara nyingi zaidi kuliko yale wanayoyafanya wale wenye hamasa na Uislam pasi na elimu ya kutosha, na wasio na msimamo. Ninaloliamini na ambalo ni deni kwangu mbele ya Allaah ni kuwa, Shaykh Muhammad Naaswirud-Diyn Al-Albaaniy, ni katika waipigao msasa Dini na wanasadikishwa na neno la Mtume (صلى الله عليه وآله وسلم):

((Allaah Hutuma kwa Ummah huu mwanzoni mwa kila miaka mia mtu wa kupiga msasa mambo ya Dini Yake)).³⁴

Mwanachuoni Wa Misr Muhibud-Diyn Al-Khatwiyb (رحمه الله)

“Miongoni mwa walinganiaji wa Sunnah waliopitisha maisha yao yote kuihuisha Sunnah ni ndugu yetu Muhammad Naaswirud-Diyn Nuuh Najaatiy Al-Albaaniy.

³⁴ Imepokewa na Abu Daawuud, na imeelezwa kuwa ni sahihi na Al-'Iraaqiy na wengineo.

**Mwanachuoni Wa Hadiyth India, Shaykh ‘Abdus-Swamad
Sharafud-Diyn (رحمه الله)**

Katika moja ya barua walizokuwa wakiandikiana na Shaykh Al-Albaaniy katika masuala ya kitafiti ya Hadiyth, alikiri kuwa Shaykh Al-Albaaniy alikuwa Mwanachuoni mkubwa wa Hadiyth.

**Mwanachuoni Hamuud Bin ‘Abdillaah At-Tuwayjiriy (رحمه
الله)**

Al-Albaaniy kwa sasa ni bendera juu ya Sunnah. Kumkosoa yeye ni kama kuikosoa Sunnah. Pia katika mnasaba wa kutolewa Tuzo la Kimataifa la Mfalme Fayswal alisema: “Hakika Shaykh Naaswir ndiye anayestahiki zaidi kupewa tuzo hili kwa kuitumikia kwake Sunnah”.

Profesa Amiyn Al-Misriy (رحمه الله) Aliyekuwa Mkuu Wa Kitengo Cha Masomo Ya Juu Katika Chuo Kikuu Cha Kiislam.

Ni moja kati ya mikosi ya dunia hii kuchaguliwa watu kama sisi wenye shahada ya udaktari wa falsafa (PhD) ili kufundisha somo la Hadiyth katika Chuo Kikuu, ilhali yuko mtu anayestahiki hilo kuliko sisi kwa namna ambayo hatufai sisi kuwa ni wanafunzi wake katika taaluma hii. Lakini huu ndio mfumo ulivyo na desturi.

Na Katika Waliomsifu Baada Ya Kufa Kwake Ni:

Waziri Wa Masuala Ya Kiislamu, Al-Awqaaf, Ulinganio Na Uongozi Shaykh Swaalih Bin 'Abdil-'Aziyz Bin Muhammad Aali Shaykh

Alisema: “Shukrani ni za Allaah kwa hukumu Zake na uwezo Wake ((Hakika sisi ni wa Allaah na hakika sisi Kwake ni wenye kurejea)).³⁵ Hakuna shaka kwamba kumpoteza Mwanachuoni Mkubwa Shaykh Muhammad Naaswirud-Diyn Al-Albaaniy, ni msiba. Yeye ni katika Wanachuoni wakubwa wa Ummah na mabingwa wa Hadiyth. Kwa Ma'ulamaa hao (Shaykh Al-Albaaniy), Allaah Mtukufu Ameilinda Dini hii na Akaieneza Sunnah kupitia kwao...”

Katibu Mkuu Wa Shirikisho La Ulimwengu Wa Kiislamu Huko Makkah Al-Mukarramah Shaykh Dkt. 'Abdullah Bin Swaalih Al-'Ubayd

Hakuna shaka yoyote kwamba kufariki Shaykh Muhammad Naaswirud-Diyn Al-Albaaniy, ni hasara kubwa kwa Ummah wa Kiislam. Vielelezo vya ushahidi na michango yake ni vingi na vikubwa kupitia elimu yake katika taasisi kubwa za Kiislam kama vile Chuo Kikuu cha Kiislam Madiynah na taasisi nyinginezo kubwa za Kiislam. Shaykh Naaswir (رحمه الله), alikuwa ni mtu wa kuthaminiwa na kuheshimiwa na kila Muislam, mashirika, makundi na mataifa. Mchango wake huo, ulivikwa moja kwa kupewa Tuzo la Mfalme Fayswal kwa mchango wake mkubwa kuhusiana na tafiti zinazohusika na elimu ya Hadiyth.

³⁵ Al-Baqarah: 156

Tume Ya Kudumu Ya Tafiti Za Kitaaluma Na Utoaji Fatwa Saudi Arabia

Waliulizwa swali lifuatalo kuhusiana na Shaykh Al-Albaaniy:

SWALI: Siku hizi watu wanazungumza sana juu ya mmoja kati ya Ma'ulamaa wenye kufanya kazi ya kuinusuru Dini hii. Si mwingine bali ni Muhammad Naaswirud-Diyn Al-Albaaniy. Wanamtuhumu kwamba yeye ni mtu asiye na elimu, na ameibuka tu ili kuzusha mkorogano baina ya watu. Kuna mtu aliyesema: "Hakika mimi nimeanza kumchukia kwa ajili ya Allaah". Basi je, kazi hii anayoifanya Shaykh huyu mtukufu si kazi inayoufaa Uislam na Waislam?! Nizingatiwe kuwa mimi sina kasumba naye, kwani kumheshimu yeye hakumaanishi kwamba mimi nina kasumba kwa mtu yeyote kijingajinga tu. Tutawaambia nini watu wasemao: "Watu wanakufa huko Syria na Afghanistan na yeye bado anahangaika na Hadiyth sahihi na dhaifu. Mnatuambia nini kuhusu Ustaadh huyu?"

Wakajibu:

JIBU: Mtu huyu (Shaykh Al-Albaaniy) anajulikana kwetu kwa elimu yake, mchango wake, kuitukuza kwake Sunnah na kuitumikia. Pia anajulikana kwa kuunga kwake mkono madhehebu ya Ahlus-Sunnah wal Jama'aah katika kutahadharisha kasumba, na ufuasi bila dalili, na vitabu vyake vyenye faida. Lakini yeye kama walivyo Ma'ulamaa wengine, si mtu aliyetakaswa na makosa. Yeye hukosea na hupatia. Tunamtarajia alipwe thawabu mbili katika alilolipatia, na thawabu moja ya kujitahidi na kukosea kama ilivyothibiti toka kwa Nabii (صلی الله علیه وآله وسلم):

((Mwenye kuhukumu anapohukumu akajitahidi na akapatia, basi ana thawabu mbili, na anapohukumu akajitahidi na akakosea, basi ana thawabu moja)).

Tunamuomba Allaah Atupe tawfiyq sisi, nyinyi na yeye, tuweze kusimama imara mbele ya haki na kuepukana na upotofu wa fitna.

Kwa Allaah ndio tawfiyq. Na Rehma ziwe juu ya Nabii wetu Muhammad, Ahli zake na Maswahaba wake.³⁶

Tenzi Kumhusu Shaykh Al-Albaaniy³⁷

Hakika anayeinusu Shari'ah ya Mola wetu,
hunosuriwa kama ulivyosema wahyi.

Na hakika tumemwona mhakiki wa enzi yetu,
naye ni Mwanachuoni wa Hadiyith Naaswir Al-Albaaniy.

Ni yule ambaye wewe umekamia kumpinga,
ewe dhalimu, acha kuasi.

Watu waliokasumbika na ushabiki wa madhehebu,
na kwa Manhaj na 'Aqiydah ya kikuhani...

Watu waliokasumbika na ushabiki wa madhehebu,
na kwa kazi yenye mabaki yasiyosalia...

³⁶ *Al-Lajnatud Daaimah Lil-Buhuuth Al-'Ilmiyah wal-Iftaa*, Fatwa Namba 12/244.

³⁷ Tenzi hii asli yake ni ya Kiarabu, kufasiriwa kwake Kiswahili kumepoteza sifa ya tenzi lakini kumebakisha maana iliyokusudiwa ndani tenzi ya Kiarabu.

Hao wamedhihiri hasira zao,
kwa kutukana na kuchafua heshima za watu ardhini.

Qiyaamah chao kimewadia na wote wamesimama,
lakini Shaykh Naaswir amesimama imara.

Ameeneza elimu bora kabisa katika enzi yetu,
ameeneza Shari'ah ya Ar-Rahmaan.

Hakufanyia kasumba wala kushabikia dhehebu lolote,
bali amewasifu na kuwapa haki zao Maimaam wote waliomtakasia Ar-
Rahmaan.

Licha ya mahasidi na wenye chuki kusema ovyo,
lakini hata hivyo, Allaah Amewanufaisha watu kwa elimu yake.

Wamemsema ni mshairi, nikasema nampenda,
hususani Naaswir Al-Albaaniy.

Ni bendera ya wakati wetu, basi siwezi kuishusha na kuidharau haki
yake,

ni Shaykh wa Mashaykh, mwenye akili ya kimola.

Yeye ndiye mkarabati wa zama,

na hakika imekuja, habari sahihi inayoishilia kwa aliye karibu.

Nyakati zote yeye ni mwalimu,
anayelingania Shari'ah ya Mola wetu Ar-Rahmaan.

Yeye ndiye Imaam kama Maimaam watahesabiwa,
nina shaka kabisa, na naapa kwa Yule Aliyeniumba.

Naye ndiye amekuwa wa kipekee katika zama zake,
kwa Fiqh, Hadiyth na Qur-aan.

Ameitetea na kuipigania sana Sunnah ya Nabii Muhammad,
mteuliwa na mchaguliwa.

Ni Bid'ah ngapi alizozipiga vita,
bid'ah zilizopakaza uso wa dini yetu kwa adha na fitina.

Amelingania Tawhiyd na Ucha Mungu,
na amesema mara nyingi mfuatani Nabii wetu 'Adnaani.

Kwani hiyo ni faradhi, wajibu na lazima,
hatuwezi kuongoka tukimfuata mwengine* ikiwa twataka 'amali zifae
katika mizani.

*mwengine asiye Muhammad (صلى الله عليه وآله وسلم).

Tanbihi Kutoka Kwa Mwandishi Wa Historia Hii

Pamoja na kuwa Shaykh Al-Albaaniy (رحمه الله) alikuwa ni Mwanachuoni wa aina yake, na hoja katika Ummah katika elimu ya Hadiyith, ni muhimu tuisahau kuwa alikuwa ni mwana Adam ambaye kwa kawaida hupatia na hukosea. Hatupaswi kufanya kama wanavyofanya baadhi ya vijana wenye hamasa, kumtukuza kupita kiasi na kuchukua kila linalotoka kwake na kuona kuwa haliwezi kuwa na makosa. Na isitoshe huwakosoa hadi kugombana na wale wasiokubaliana na baadhi ya fatwa za Shaykh. Imefikia hadi baadhi ya wanafunzi na vijana kuwaponda Wanachuoni wengine kwa sababu tu wana rai inayotofautiana na Shaykh (رحمه الله). Huo si msimamo wa haki, na pia si msimamo wa Shaykh mwenyewe. Shaykh (رحمه الله) alikuwa akipokea haki na dalili japo ziko dhidi yake maadam ni sahihi kuliko zake.

Hatutoweza kumsahau kwa wepesi Shaykh wetu huyu mtukufu, kwa elimu yake inayowanufaisha mamilioni leo hii na itakayowanufaisha vizazi kwa vizazi hadi siku ya mwisho. Allaah Amrehemu na Amwandalie nyumba bora huko katika pepo Yake ya Firdaws. Aamiyn

**Mitandao Iliyoundwa Kwa Ajili Ya Kueneza Elimu Shaykh
Al-Albaaniy (رحمه الله)**

Mawaidha Na Fataawa Za Shaykh

http://www.alalbany.net/albany_tapes.php

Mtandao Kwa Lugha Ya Kiarabu

<http://www.alalbany.net/>

Mitandao Kwa Lugha Ya Kiingereza

http://www.alalbany.net/albany_eng.php

<http://www.albani.co.uk>

<http://www.twtpubs.com/web/>

<http://www.shaikhalbaani.wordpress.com>